

### 3. Misimu

Tazama picha na maelezo ya misimu, kisha jibu maswali (a), (b) na (c).

- A.** Huu ni wakati wa kiangazi, yaani, jua kali. Wakulima wanatayarisha mashamba yao.



- B.** Huu ni msimu wa masika. Watu wamekwisha kupanda nafaka. Miche ya nafaka imechipuza. Ni wakati wa radi, mingurumo na mvua nyingi.



- C.** Huu ni msimu wa kipupwe. Kuna baridi wakati huu. Msimu huu huja baada ya msimu wa masika.



- D.** Huu ni msimu wa vuli. Kuna mvua nyepesi wakati huu. Baada ya mvua za vuli, huingia wakati wa kiangazi.



**Jibu maswali haya:**

- Nini tofauti baina ya Picha A na Picha B?
- Baridi nyingi huwa katika msimu gani?
- Ni msimu gani wenye mvua za rasharasha, yaani mvua nyepesi?